TANZANIA COALITION ON DEBT AND DEVELOPMENT (TCDD)

HALI YA ELIMU YA SEKONDARI KATIKA MAZINGIRA YA ELIMU BILA MALIPO NCHINI TANZANIA

MWAKA 2017



DESEMBA 2017

YALIYOMO

Shukrani ……iii
Vifupisho …… iv

SURA YA KWANZA
UTANGULIZI…… 1

1.0. MSINGI WA MRADI WA UTAFITI …… 1
1.1. Ushiriki wa asasi za Kiraia katika maendeleo …… 1
1.2. Njia za Utafiti…… 2
1.3. Sampuli…… 2
1.4. Zana za ukusanyaji takwimu …… 2
1.5. Baadhi ya mambo muhimu yaliyoangaliwa kwenye utafiti huu …… 2

SURA YA PILI
2.0. MATOKEO YA UTAFITI KATIKA SEKTA YA ELIMU…… 3
2.1. Halmashauri na Idadi ya shule zilizohusika kwenye utafiti…… 3
2.2. Jumla ya wanafunzi walioandikishwa kidato cha Kwanza mwaka 2015 na 2016…… 3
2.3. Wanafunzi ambao hawakuripoti shuleni baada ya kuchaguliwa…… 5
2.4. Idadi ya wanafunzi waliofanya mtihani wa Kidato cha Nne na waliofaulu…… 6
2.5. Idadi ya wanafunzi waliojiunga kidato cha tano…… 8
2.6. Uwiano wa Idadi ya Walimu na Wanafunzi katika Wilaya kwa somo…… 9
2.7. Uwiano wa wanafunzi kwa kila chumba cha Darasa/ujazo wa wanafunzi …… 12
2.8. Uwiano wa Idadi ya wanafunzi kwa matundu ya vyoo katika Halmashauri …… 17
2.9. Shule zenye umeme …… 21

SURA YA TATU
UFUATILIAJI WA MRADI WA 2014/2016 (BACK STOPPING) …… 25
3.0. UTANGULIZI …… 25
3.1. Sekta ya Elimu …… 25
3.2. Halmashauri zilizohusika …… 25
3.3. Jumla ya wanafunzi walioandikishwa kidato cha kwanza 2015 na 2016…… 25
3.4. Wanafunzi waliochaguliwa na hawakuripoti shuleni …… 27
3.5. Idadi ya wanafunzi waliofanya mtihani wa kidato cha nne na waliofaulu …… 30
3.6. Uwiano wa idadi ya walimu na wanafunzi …… 33
3.7. Uwiano wa wanafunzi na matundu ya vyoo …… 35

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na 1: Idadi ya shule zilizohusika kwenye utafiti…… 3

Jedwali Na 2: Jumla ya Wanafunzi walioandikishwa Kidato cha Kwanza …… 4

Jedwali Na 3: Wanafunzi ambao hawakuripoti shule baada ya kuchaguliwa …… 4

Jedwali Na 4: Takwimu kutoka katika shule 10 kila Wilaya…… 6

Jedwali Na 5: Idadi ya wanafunzi waliojiunga kidato cha tano (5) …… 9

Jedwali Na 6: Uwiano wa Idadi ya Walimu na wanafunzi katika wilaya/Halmashauri kwa somo 9

Jedwali Na 7: Uwiano wa Idadi ya wanafunzi kwa matundu ya vyoo katika Halmashauri 17

Jedwali Na 8: Shule zenye umeme …… 21

ORODHA YA PICHA

Picha Na.1 na 2: Uwiano wa wanafunzi kwa kila chumba cha darasa: (Toangoma sekondari na Wailes sekondari: Manispaa ya Temeke……..... 16

Picha Na 3 na 4: Nyansha sekondari na Pogwe sekondari: wilaya ya Kasulu…..... 16

Picha Na 5 na 6: Hali halisi ya Vyoo vinavyotumika: Manispaa ya Temeke Dar es salaam ……..... 18

Picha Na 7 na 8: Hali halisi ya vyoo vinavyotumika: Wilaya ya Lushoto ……..... 19

Picha Na 9 na 10: Hali halisi ya vyoo vinavyotumika katika picha: Wilaya ya Kasulu - Mbono sekondari……..... 20

Picha Na 11 na 12: Mrufi sekondari, Kasulu Kigoma……..... 20

Picha Na 13 na 14: Choo cha wavulana, sabasaba sekondari - Mtwara Mikindani.... 21

Picha Na 15 na 16: Maabara (Kabuhoro sekondari na Nyamanoro sekondari - Ilemela, Mwanza……..…… 22

Picha Na 17 na 18: Pasiansi sekondari na Nyumbigwa sekondari……..…… 22

Picha Na 19: Jiko: Malela sekondari, Manispaa ya Temeke……..…… 22

Picha Na 20: Darasa, sekondari uwanja wa Taifa Morogoro Manispaa……..… 23

Picha Na 21 Na 22: Shule ya sekondari Hwazi - Kasulu, Kigoma……..… 23

SHUKRANI

Kitabu hiki cha hali ya Elimu na changamoto zake nchini Tanzania ni mwendelezo wa tafiti ambazo Mtandao wa Madeni na Maendeleo Tanzania (TCDD) imekuwa ikizifanya tangu mwaka 2001 katika sekta za afya na elimu. Kitabu hiki kinaainisha hatua zote za mchakato mzima wa ufuatiliaji, umuhimu, malengo, njia, sampuli na zana za utafiti. Kitabu pia kinatoa matokeo ya utafiti kwenye Halmashauri kumi (10) ambapo utafiti huu umejikita katika kufuatilia utekelezaji wa mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (5) 2016/2017 – 2020/2021 katika Halmashauri za Mtwara (Manispaa), Morogoro (Manispaa), Ilemela, Temeke, Singida (Manispaa), Kasulu, Urambo, Arumeru Magharibi (Arusha DC), Mbeya Vijijini (Mbeya DC) na Lushoto. Kitabu hiki kinachambua matokeo kutoka katika shule za Sekondari 100 yaani shule 10 kutoka katika kila Wilaya teule hapo juu kama sampuli wakilishi ya sekta nzima katika Halmashauri hizo.

Shukrani za dhati ziwaendee wote waliohusika kikamilifu katika kukamilisha kazi hii Kama ifuatavyo; Wakurugenzi watendaji wa Halmashauri zote ambazo zimehusika kikamilifu katika utafiti huu, wakuu wa wilaya zote, maafisa elimu wa wilaya, walimu wakuu pamoja na wazazi wote ambao walihusika kwa ukaribu kafanikisha zoezi hili.

Kwa namna ya pekee tunapenda kuyashukuru mashirika wanachama wa TCDD hasa yaliyohusika kikamilifu katika utafiti huu katika Wilaya zao ambayo ni; Sustainable Environment Management Action (SEMA), Community Active in Development Association (CADA), Hands for Children and Women Tanzania (HACHAWOTA), Mtwara Non Government Network (MTWANGONET), The National Network for Advancement (NIA), TULEANE Group, TUSHIRIKI, Union of Non Governmental Organisation (UNGO), Baraza la Kuratibu na Kukuza Maendeleo na Mahusiano ya Kijamii Kijinsia (WEGCC), Youth Peace Makers (YPM).

Shukrani pia zimwendee Ndugu Boniface Komba ambaye amesaidia kuweka pamoja taarifa za Halmashauri zote 10 na kuwa taarifa moja, Ndugu Jane Mwabulambo ambaye pia amefanya kazi ya kuboresha kitabu hiki katika hatua zote. Wote kwa ujumla wao walitoa mchango mkubwa katika kuboresha na kuchapisha kitabu hiki ambacho sio tu kwamba kitawasaidia watanzania na watunga sera kwa ujumla bali kitumike kama sehemu ya ushawishi na utetezi/uchechemuzi katika kuboresha huduma ya elimu ya sekondari kwa nchi nzima.

Hebron Mwakagenda
Mkurugenzi Mtendaji
Disemba 2017

TANZANIA COALITION ON
DEBT AND DEVELOPMENT
(TCDD)
P. O. Box 80147
DAR ES SALAAM, TANZANIA

VIFUPISHO

TCDD	Tanzania Coalition on Debt and Development
MKUKUTA II	Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini Tanzania Awamu ya Pili
SEMA	Sustainable Environment Management Action
CADA	Community Active in Development Association
HACHAWOTA	Hands for Children and Women Tanzania
MTWANGONET	Mtwara Non Governmental Organization Network
NIA	The National Intergity for Advancement (NIA)
UNGO	Union of Non Governmental Organisation (UNGO)
WEGCC	Baraza la Kuratibu na kukuza maendeleo na mahusiano ya kijamii kijinsia
YPM	Youth Peace Makers
HT	Hakuna Taarifa

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.0. MSINGI WA MRADI WA UTAFITI

Umaskini ni miongoni mwa changamoto kubwa inayoikabili Tanzania na nchi nyingine nyingi zinazoendelea hasa zilizopo chini ya ukanda wa jangwa la sahara, hii ni pamoja na kuwepo kwa taarifa zinazoashiria kuimarika na kukua kwa uchumi wa Tanzania kwa wastani wa asilimia 6.8 hadi 7 kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kuelekea asilimia 10 kwa mwaka ikiwa ni lengo mojawapo la mpango wa pili wa Taifa wa maendeleo kufikia 2021. Sababu nyingi zimekuwa zikielezwa kupelekea hali hii ya umaskini hapa nchini ambazo ni pamoja na Sera za Uchumi: Sera za fedha na matumizi ya Serikali kutotosheleza kukuza uchumi unaonufaisha wengi, Huduma zisizotosheleza katika sekta ya kilimo, Uwekezaji usiotosheleza katika viwanda mijini na vijijini, Teknolojia duni, Mila potofu na desturi zisizo na tija katika kuleta maendeleo (ubaguzi wa kijinsia; ushirikina) na Kuwa na deni kubwa la Taifa.

Katika jitihada za kupunguza na kuondoa umaskini, Tanzania imeanzisha mikakati ya makusudi ambayo ni mwongozo wa maendeleo ya jamii na uchumi. Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inatamka kuwa Tanzania itakuwa imefuta umaskini ifikapo mwaka 2025 ambapo Tanzania itakuwa imefikia kiwango cha kati cha maendeleo. Katika kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Tanzania ilitengeneza na kutekeleza mkakati maalum wa muda ambao ni Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA II) 2010/2011 – 2014/2015 na hivi sasa Mpango wa pili wa maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/2017 – 2020/2021 lengo likiwa kufikia matarajio ya Dira ya taifa na malengo ya milenia.

Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/2017 – 2020/2021 umejikita hasa katika ukuaji wa viwanda vitakavyochochea mabadiliko ya uchumi na maendeleo ya watu kufikia uchumi wa kati wa viwanda na kuwa na watu wenye ujuzi watakaochochea ukuaji wa uchumi kwa kuhakikisha Sekta zinazoajiri watu wengi na walio masikini zinakuwa kwa kasi. Lengo likiwa ifikapo mwaka 2025, Tanzania iwe nchi yenye maisha bora, yenye amani, umoja na utawala bora, jamii inayojifunza na iliyoelimika, yenye uwezo wa kuzalisha na kuwa na ukuaji wa uchumi endelevu na wenye ushindani

1.1. Ushiriki wa Asasi za Kiraia katika Maendeleo

Katika kukuza ufanisi na utekelezaji makini wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/2017 – 2020/2021 usimamizi ni suala muhimu hasa pale mpango huu unapojikita katika kuboresha maisha na ustawi wa jamii hasa kwa watu walio maskini zaidi pamoja na wale walio katika mazingira hatarishi.

Usimamizi mzuri ni pamoja na upatikanaji wa taarifa sahihi kwa muda muafaka na ili kufanikisha upatikanaji wa taarifa sahihi kwa wakati, serikali kupitia mfumo wake wa kitaifa wa usimamiaji wa programu ya kupunguza umaskini, inahimiza usimamizi shirikishi wa asasi za kiraia. Katika muktadha huo, TCDD imejikita katika mradi wa kukusanya takwimu, taarifa na vielelezo vitakavyosaidia ufikiwaji wa maamuzi na uimarishaji wa uwezo wa asasi zisizo za kiserikali ziweze kujihusisha kwa usahihi zaidi katika majadiliano ya kisera lakini pia kuangalia utekelezaji, ufuatiliaji, na tathmini ili kujiridhisha na ufanisi wa Mpango wa pili wa maendeleo wa Taifa wa Miaka mitano 2016/2017 – 2020/2021 kwa jamii ya Tanzania kuelekea katika Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025.

Malengo ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/2017 – 2020/2021 yanaweza kufikiwa tu endapo wadau mbalimbali wa maendeleo watashiriki kikamilifu katika utekelezaji wake. Wadau wa Maendeleo sio wale tu walio katika taasisi za Kiserikali na Bunge, bali pia walio katika asasi za kijamii, sekta binafsi, wafadhili na jamii yote kwa ujumla. Wadau wanahimizwa kushiriki kikamilifu katika utekelezaji ili kujenga hamasa na hali ya umiliki wa mpango huu kwa jamii.

1.2. Njia za Utafiti

Utafiti huu ulihusisha ukusanyaji wa taarifa kutoka kwa wadau mbalimbali wa elimu juu ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/2017 – 2020/2021 katika wilaya 10 pendekezwa na kujionea hali halisi kwa kutazama kiwango cha utekelezaji wa miradi mbalimbali katika Sekta ya Elimu ikihusisha viashiria vya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/2017 – 2020/2021 katika sekta hiyo.

1.3. Sampuli

Sampuli iliyotumika katika utafiti huu zilipatikana kutokana na mapendekezo yaliyotokana na wadau na wanachama wa TCDD. Kila Halmashauri ilichagua shule zisizopungua Kumi za Sekondari katika utafiti huo ambako taarifa zilikusanywa katika ngazi ya shule na ngazi ya Halmashauri. Halimashauri zilizohusika kwenye utafiti/ufuatiliaji huu ni; Manispaa ya Temeke- Dar es salaam, Manispaa ya Mtwara, Manispaa ya Morogoro, Ilemela-Mwanza, Kasulu – Kigoma, Urambo-Tabora, Arumeru Mashariki-Arusha, Mbeya Vijijini, Manispaa ya singida na Lushoto-Tanga.

1.4. Zana za ukusanyaji takwimu

Takwimu zilikusanywa kwa kutumia madodoso na majadiliano vikundini. Madodoso yalijumuisha maswali ya wazi na yasiyo ya wazi kwa Halmashauri zote. Madodoso hayo yalikuwa yamegawanyika katika sehemu kuu tatu nazo ni madodoso kwa wakuu wa shule za sekondari, madodoso kwa Maafisa Elimu Halmashauri, na madodoso ya namna ya uendeshaji wa majadiliano kwa vikundi ambayo yaliendeshwa kwa kushirikisha kamati za shule katika ngazi mbalimbali za Halmashauri husika, wazazi na wanafunzi.

1.5. Baadhi ya mambo muhimu yaliyoangaliwa kwenye utafiti huu

Uwiano wa wanafunzi kwa vitabu (kiada), walimu, madarasa, madawati, miundombinu nk, ufaulu wa wanafunzi, uwajibikaji wa jamii katika suala zima lihusulo elimu kwa watoto hasa watoto wa kike. Hii ikiwa ni sehemu ya kupima kama malengo Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/2017 – 2020/2021 katika sekta ya Elimu yanaendelea kufikiwa. Lakini pia utafiti huu unasaidia kubaini baadhi ya changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa Mpango huo wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/2017 – 2020/2021 katika sekta ya hiyo.

SURA YA PILI

2.0. MATOKEO YA UTAFITI KATIKA SEKTA YA ELIMU YA SEKONDARI

Elimu ni moja ya sekta muhimu ambayo Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/2017 – 2020/2021 umejizatiti katika kuondoa changamoto zinazoikabili ili kuleta ustawi wa Taifa la Tanzania. Mpango unaainisha changamoto kadha wa kadha kama vile upungufu wa walimu na uwepo wa walimu wasio na ubora, mazingira yasiyo rafiki ya kujifunzia, upungufu wa madarasa na vyoo vya wanafunzi, upungufu wa walimu na vitabu kwa masomo ya sayansi na kiwango kidogo cha wanafunzi wanaofaulu na kujiunga na masomo ya kidato cha tano.

Moja ya matarajio makubwa katika sekta hii ya elimu ni kuongeza uwezekano wa wananchi wengi kuwa na fursa ya kupata elimu bora katika ngazi mbalimbali, hasa katika elimu ya msingi na sekondari. Kwa kuzingatia viashilia vilivyotolewa kwenye mpango katika sekta ya Elimu Jumla ya Halmashauri 10 zilihusishwa katika utafiti huu ambazo ni Mtwara Manispaa, Morogoro Manispaa, Ilemela, Temeke, Singida Manispaa, Kasulu, Urambo, Mbeya Vijijini (Mbeya DC), Arumeru Magharibi (Arusha DC) na Lushoto. Jumla ya shule za serikali 100 hasa shule za kata zilitarajiwa kuhusika katika utafiti huu, lengo likiwa ni kutembelea shule 10 za sekondari kutoka katika kila Halmashauri husika.

2.1. Halmashauri na Idadi ya shule zilizohusika katika utafiti huu

Jedwali Na 1: Idadi ya shule zilizohusika kwenye utafiti.

	Halmashauri	Idadi ya Shule	Wilaya	Idadi ya Shule
1.	Mtwara Manispaa	10	Urambo	10
2.	Morogoro Manispaa	10	Mbeya vijijini	10
3.	Ilemela Manispaa	10	Arumeru Magharibi	10
4.	Temeke Manispaa	10	Lushoto	10
5.	Singida Manispaa	10	Kasulu	10

Chanzo: Utafiti 2017

2.2. Jumla ya Wanafunzi walioandikishwa kidato cha kwanza mwaka 2015 na 2016

Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka mitano 2016/2017 – 2020/2021 unaainisha hali halisi ya uandikishaji kwa mwaka 2014/2015 ambao ni 41% kwa elimu ya sekondari ya chini, lengo likiwa 43% kufikia 2020/21. Utafiti huu unabainisha hali halisi kutoka uwandani juu ya hali ya uandikishaji wa wanafunzi wa kidato cha kwanza kutoka katika shule 100 zilizotembelewa katika wilaya 10.

Jedwali Na.2: Jumla ya Wanafunzi walioandikishwa

Mwaka	2015			2016			
Halmashauri	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla	Jumla Kuu
Mtwara Manispaa	505	549	**1054**	570	698	**1268**	**2322**
Morogoro Manispaa	1052	1054	**2136**	1144	1262	**2387**	**4523**
Ilemela	880	1008	**1886**	1247	1102	**2349**	**4235**
Temeke	1531	1853	**3382**	1621	2509	**4130**	**7512**
Singida	382	475	**857**	504	598	**1102**	**1959**
Urambo	505	406	**911**	559	497	**1056**	**1967**
Mbeya vijijini	627	777	**1404**	833	874	**1707**	**3111**
Arumeru Magharibi	786	965	**1751**	977	1255	**2232**	**3983**
Kasulu	499	425	**924**	788	460	**1248**	**2172**

Takwimu kutoka katika wilaya 10 ambazo utafiti huu umefanyika zinaonyesha ongezeko kubwa la wanafunzi wa kidato cha kwanza walioandikishwa kwa mwaka 2015 na 2016 kama inavyoonekana kwenye jedwali. Pia udahili wa wanafunzi wa jinsi ya kike katika wilaya zote isipokuwa wilaya ya Kasulu umeongezeka ikilinganishwa na jinsi ya kiume. Kwa mujibu wa tafiti, ongezeko hili limechangizwa na uwepo wa elimu bila malipo (karo ya shule) na michango mbalimbali ambayo ilionekana kuwa ni mzigo kwa wazazi lakini pia ongezeko la wanafunzi wanaofaulu darasa la saba.

Grafu Na 1: Kuongezeka Kwa wanafunzi wa jinsi ya kike walioandikishwa kidato cha kwanza mwaka 2015 na 2016



Chanzo: Utafiti 2017

TCDD inashauri kuwa ongezeko hili la idadi ya wanafunzi wanaojiunga kidato cha kwanza liende sambamba na ongezeko na maboresho ya miundombinu itakayowezesha upatikanaji wa elimu bora katika mazingira bora kama vile mabweni (hasa kwa watoto wa kike), maabara, madarasa, vyoo, maji, umeme, vitabu na hata nyumba za walimu.

Utafiti huu umeainisha changamoto kadhaa ambazo zimeathiri uandikishaji wa wanafunzi wa kidato cha kwanza kama vile;

- Mimba kwa wanafunzi wa kike
- Hali ngumu ya Maisha kwa wazazi
- Mwamko duni wa wazazi juu ya umuhimu wa Elimu.

2.3. Wanafunzi ambao hawakuripoti shuleni baada ya kuchaguliwa

Takwimu zinaonyesha kuwepo kwa idadi kubwa ya wanafunzi ambao hawakuripoti katika shule walizopangiwa kwaajili ya masomo ya kidato cha kwanza Kwa mwaka 2015 na 2016 kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini; Hili ni tatizo endapo mamlaka husika haitachukua hatua za kutosha ili kudhibiti tatizo hili;

Jedwali Na 3: Wanafunzi ambao hawakuripoti shuleni baada ya kuchaguliwa

MWAKA	2015		Jumla	2016		Jumla
WILAYA	Me	Ke		Me	Ke	
Mtwara Manispaa	52	80	**132**	43	70	**113**
Morogoro Manispaa	252	174	**426**	146	152	**298**
Ilemela Manispaa	195	162	**252**	175	178	**353**
Singida Manispaa	29	37	**66**	18	44	**62**
Urambo Manispaa	72	56	**128**	44	49	**93**
Mbeya Vijiji	125	157	**282**	142	158	**300**
Arumeru Magharibi	224	327	**571**	237	229	**466**
Kasulu	47	107	**154**	108	95	**203**



Chanzo: utafiti 2017

Kuna sababu mbalimbali kutoka katika shule zilizofanyiwa utafiti ambazo zinatajwa kupelekea kusababisha wanafunzi kutokuripoti mara wanapochaguliwa kujiunga nazo, kama ifuatavyo:

- Baadhi ya wanafunzi kujiunga na shule za taasisi binafsi (private schools)
- Utoro unaosababishwa na baadhi ya wanafunzi kujingiza kwenye biashara ndogondogo na biashara ya bodaboda kwa vijana wa kiume.
- Mwamko mdogo wa Elimu kutoka kwa wazazi na jamii kwa ujumla
- Shughuli za kilimo, ufugaji, uvuvi, machimbo madogomadogo
- Mimba Kwa watoto wa kike na
- Hali ya umaskini kwa wazazi.

Kwenye jamii za kifugaji kama vile Arumeru Magharibi ambako utafiti huu pia umefanyika, wazazi wengi wamekosa mwamko wa elimu hivyo kuwaruhusu watoto wao kushughulika na uchungaji wa ng'ombe kuliko kuendelea na elimu. Pia kuwepo kwa mila na tamaduni ambazo zinahamasisha wasichana kuolewa katika umri mdogo.

2.4. Idadi ya Wanafunzi waliofanya Mtihani wa kidato cha Nne na Waliofaulu

MWAKA		2015				2016			
Halmashauri	WATAHINIWA	Me		Ke		Me		Ke	
Mtwara Manispaa	Watahiniwa	513	50%	518	50%	492	52%	460	48%
	waliofaulu	302	29%	282	27%	273	28%	543	57%
Morogoro Manispaa	Watahiniwa	850	49%	881	51%	887	49%	930	51%
	waliofaulu	436	25%	483	28%	489	27%	484	26%
Ilemela	Watahiniwa	1990	51%	1946	49%	1174	50%	1177	50%
	waliofaulu	1005	25%	1038	26%	882	38%	881	37%
Temeke	Watahiniwa	1225	46%	1422	54%	1225	45%	1488	55%
	waliofaulu	767	29%	643	24%	624	23%	614	23%
Singida Manispaa	Watahiniwa	402	48%	430	52%	359	44%	454	56%
	waliofaulu	258	31%	265	32%	208	26%	270	33%
Urambo	Watahiniwa	304	55%	251	45%	240	51%	228	49%
	waliofaulu	184	33%	118	21%	185	40%	109	23%
Mbeya vijijini	Watahiniwa	631	47%	721	53%	645	46%	768	54%
	waliofaulu	360	27%	398	29%	236	17%	434	31%
Arumeru Magharibi	Watahiniwa	673	39%	1041	61%	679	40%	1052	61%
	waliofaulu	466	27%	604	35%	452	38%	725	62%
Kasulu	Watahiniwa	567	57%	425	43%	419	57%	311	43%
	waliofaulu	354	64%	195	36%	241	33%	187	26%

Jedwali Na 4: Takwimu kutoka katika Shule kumi (10) kila wilaya

Jedwali hapo juu linaonyesha idadi ya watahiniwa kutoka katika shule kumi (10) zilizofanyiwa utafiti na wanafunzi waliofaulu kwa mwaka 2015 na 2016. Takwimu zinaonyesha hali ya ufaulu kuwa usioridhisha na juhudi za makusudi zisipochukuliwa mapema ni ngumu kufikia lengo la ufaulu kutoka 69.8% kwa mwaka 2014/2015 hadi 80% mwaka 2020/21 na 90% mwaka 2025/26. Takwimu zinaonyesha karibia nusu ya watahiniwa wanaofanya mtihani katika shule mbalimbali hawafaulu mitihani yao ili waweze kuendelea na masomo ya kidato cha tano.

TAKWIMU ZA KIWILAYA KUTOKA KATIKA OFISI ZA ELIMU MANISPAA NA HALMASHAURI ZA WILAYA nazo zinaonyesha hali ya ufaulu usioridhisha katika maeneo mbalimbali Kama inavyoonekana kwenye majedwali yafuatayo ukurasa unaofuata;-

Manispaa ya Mtwara Mikindani

Mwaka	2015			2016		
Jinsi	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla
Watahiniwa	881	793	1674	802	938	1740
Waliofaulu	570	478	1048	543	665	1208



Manispaa ya Temeke

Mwaka	2015			2016		
Jinsi	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla
Watahiniwa	4649	5131	9780	4518	5264	9782
Waliofaulu	2262	2542	4804	3522	3815	7337



Wilaya ya Lushoto

Mwaka	2015			2016		
Jinsi	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla
Watahiniwa	1769	1838	3607	1133	1968	3101
Waliofaulu	841	1339	2240	748	1218	1966
%	48	72	62	66	62	63



Kwa ujumla, takwimu kutoka katika shule kumi (10) zilizotembelewa na Elimu Wilaya/ Halmashauri zinabainisha hali ya ufaulu kuwa chini ukilinganisha na idadi ya watahiniwa wote, huku hali ya ufaulu kwa kuzingatia jinsi ya kike na kiume ikionyesha kuto-tofautiana sana.

Pamoja na sababu tajwa hapo chini, kupungua kwa idadi ya wanaofaulu kunatokana na kutokuwepo kwa mazingira rafiki ya upatikanaji wa elimu bora ikiwemo uchache wa walimu hasa wa sayansi, Mfano; shule ya sekondari Chuno, Manispaa ya Mtwara Mikindani haina mwalimu wa Sayansi, ukosefu wa vitendea kazi kama vile vitabu, uchache wa vyumba vya madarasa, madawati na kukosekana kwa vitendea kazi katika maabara. Kati ya shule 10 zilizotajwa kuwa na maabara katika Manispaa ya Mikindani ni shule 2 tu ndizo maabara zinafanya kazi ingawa nazo hazijakamilika kwa asilimia mia moja.

Changamoto zingine ni;

- Utoro wa wanafunzi.
- Uhaba wa walimu; hasa wa masomo ya sayansi.
- Ushiriki hafifu wa wazazi katika kufuatilia maendeleo ya watoto wao.
- Mazingira yasiyo rafiki ya kujifunzia, kama vile ubovu wa vyoo, upungufu wa vyumba vya madarasa, mabweni hasa kwa wanafunzi wa jinsi ya kike, kukosekana kwa maabara, madawati, nk.
- Kuwepo kwa mila na desturi zinazofifisha maendeleo ya elimu hasa kwa watoto wa kike.
- Mimba na ndoa za utotoni
- Kukata tamaa kwa walimu kutokana na baadhi ya mazingira ya kazi kuwa magumu, kutopewa motisha na uhaba wa vitendea kazi.

2.5. Idadi ya wanafunzi waliojiunga kidato cha tano (5)

Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/2017 – 2020/2021 unalenga Kuongeza idadi ya wanafunzi wanaojiunga kidato cha tano (5) kutoka 10.5% mwaka 2014/2015 kufikia asilimia 20% kwa mwaka 2020/21. Jedwali hapa chini linaonyesha hali halisi kutoka katika wilaya tisa (9) kati ya kumi (10) zilizotembelewa – kwa kuzingatia hali ya ufaulu kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapa chini.

Ukilinganisha takwimu za wanafunzi waliofanya mtihani wa kidato cha nne na waliofaulu kwa mwaka 2015 na 2016 na takwimu za wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha tano kwa miaka hiyo unaweza kuona hali halisi ya idadi ndogo sana ya wanafunzi

wanaojiunga na masomo ya kidato cha tano. Idadi kubwa ya wanafunzi wanashindwa kupata alama za ufaulu ili waweze kuendelea na masomo ya kidato cha tano. Juhudi za pamoja kati ya serikali, wazazi na wadau wa elimu katika kutatua changamoto mbalimbali kama vile uhaba wa vyumba vya madarasa, ushirikiano mdogo kati ya uongozi wa shuel na wazazi au jamii,uhaba wa vifaa vya maabara na wataalamu wake, uhaba wa walimu wa masomo ya sayansi na hisabati, utoro wa wanafunzi, baadhi ya wazazi kuwaozesha watoto wa kike, jamii kutothamini elimu kutokana na uelewa mdogo wa umuhimu wa elimu kwa watoto pamoja na mazingira duni ya kuishi na kufanyia kazi kwa walimu.

Jedwali Na 5: Idadi ya wanafunzi waliojiunga kidato cha tano

MWAKA	WATAHINIWA	2015		2016	
WILAYA	WATAHINIWA	Me	Ke	Me	Ke
Mtwara Manispaa	Waliojiunga	179	517	112	265
	Walioshindwa kujiunga	19	32	16	20
Morogoro Manispaa	Waliojiunga	79	346	87	311
	Walioshindwa kujiunga	0	0	0	0
Ilemela Manispaa	Waliojiunga	144	487	180	420
	Walioshindwa kujiunga	23	32	-	27
Temeke Manispaa	Waliojiunga	370	199	426	260
	Walioshindwa kujiunga	1892	2343	3096	3555
Singida Manispaa	Waliojiunga	HT	HT	HT	HT
	Walioshindwa kujiunga	HT	HT	HT	HT
Urambo	Waliojiunga	98	17	0	0
	Walioshindwa kuiunga	467	312	0	0
Mbeya vijijini	Waliojiunga	126	123	192	166
	Walioshindwa kujiunga	46	36	76	66
Lushoto	Waliojiunga	235	574	229	290
	Walioshindwa kujiunga	606	825	519	928
Kasulu	Waliojiunga	341	124	0	0
	Walioshindwa kujiunga	0	0	0	0

Takwimu: Elimu Wilayani/Halmashauri

2.6. Uwiano wa idadi ya walimu na wanafunzi katika Wilaya/Halmashauri kwa somo

Takwimu: Elimu Wilaya/Halmashauri

Halmashauri	WALIMU		WANAFUNZI		UWIANO	UWIANO
Mtwara Manispaa Mikindani	2015	2016	2015	2016	2015	2016
	397	398	5458	5676	1:14	1:14
Morogoro Manispaa	1299	1299	15611	15313	1:12	1:12
Ilemela	847	906	16934	16834	1:20	1:18
Temeke Manispaa	1675	1718	43363	42724	1:26	1:25
Urambo	281	274	7045	4446	1:25	1:16
Mbeya	718	714	10982	10393	1:15	1:15
Lushoto	721	831	12467	12772	1:17	1:15
Kasulu	-	-	-	-	1:26	1:26

Jedwali Na 6: Uwiano wa idadi ya walimu na wanafunzi katika wilaya/Halmashauri kwa somo

Utafiti ulilenga kubaini uwiano halisi uliopo kati ya Walimu kwa wanafunzi kwa somo katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa miaka mitano unalenga kufikia uwiano wa 20:1 kufikia mwaka 2020/21 na 2025. Katika Halmashauri zilizofanyiwa utafiti, Takwimu zilizoainishwa hapo juu ni Uwiano wa kiujumla kwa halmashauri ambazo zinaonyesha mwelekeo mzuri kuelekea uwiano 20:1 kwa somo takwimu zifuatazo hapa chini ni hali halisi kutoka katika shule 10 zilizotembelewa kwa kila Halmashauri moja moja.

UWIANO WA WALIMU KWA WANAFUNZI KUTOKA KATIKA BAADHI YA HALMASHAURI 10 NA SHULE ZILIZOTEMBELEWA

Mtwara Manispaa

Jina la shule	Mwaka 2015			Mwaka 2016		
	Wanafunzi	Walimu	Uwiano	Wanafunzi	Walimu	Uwiano
Mitengo	180	17	11:1	252	17	15:1
Mangamba	181	28	7:1	168	25	7: 1
Sabasaba	600	41	15:1	549	41	14:1
Chuno	438	30	15:1	402	30	13:1
Shangani	504	32	16:1	438	32	14:1
Umoja	472	28	17:1	432	28	15:1
Rahaleo	456	29	16:1	442	29	15:1
Naliendele	371	27	14:1	386	28	14:1
Sino	493	32	15:1	479	32	15:1
Mikindani	168	19	9:1	258	19	14:1

Kwa kuzingatia lengo la mpango ambao ni 20:1 kufikia mwaka 2021, utafiti unaonyesha uwiano kuwa ni mzuri hasa kwa walimu wa masomo ya sanaa. **Changamoto kubwa** ni kwa walimu wa masomo ya sayansi, **Mfano, *Shule ya Sekondari Chuno* hakuna mwalimu wa fizikia mwalimu mkuu analazimika kufundisha somo hilo mara chache anapopata nafasi** au mwalimu yoyote ambaye walau ana uelewa kidogo wa somo hilo hali hii imepelekea matokeo mabaya ya kidato cha nne katika masomo ya sayansi.

Wilaya/Halmashauri ya Lushoto

Shule	Mwaka 2015			Mwaka 2016		
	Wanafunzi	Walimu	Uwiano	Wanafunzi	Walimu	Uwiano
B.Mshangama	162	16	10:1	181	16	11:1
Gare	223	12	19:1	190	18	11: 1
Kisaba	341	30	11:1	390	31	13:1
Kitala	192	19	10:1	180	19	10:1
Masange	310	17	18:1	392	18	22:1
Ngazi	174	16	11:1	214	16	13:1
Ngulwi	171	32	5:1	172	32	5:1
Prince Claus	188	19	10:1	172	20	9:1
Shita	229	15	15:1	274	16	17:1
Ubiri	611	31	20:1	502	24	21:1

Takwimu hapo juu zinaonyesha kuwa uwiano wa wanafunzi kwa walimu kwa kila shule katika shule zilizofanyiwa utafiti ni mzuri kwa mujibu wa sera ya elimu kwa shule za sekondari japokuwa idadi kubwa ya walimu hawa ni wa masomo ya sanaa.

Manispaa ya Temeke

Shule	Mwaka 2015			Mwaka 2016		
	Wanafunzi	Walimu	Uwiano	Wanafunzi	Walimu	Uwiano
Pendamoyo	351	12	29:1	338	12	28:1
Miburani	338	13	26:1	325	13	25:1
Wailes	421	8	52:1	386	8	48:1
Saku	323	9	35:1	357	10	36:1
Malela	225	38	5:1	336	38	8: 1
changanyikeni	206	9	22:1	286	9	31:1
Mikwambe	239	10	23:1	224	10	22:1
Toangoma	263	11	23:1	308	10	31:1
Tandika	455	18	25:1	456	19	24:1
Lumo	306	9	34:1	322	10	32:1

Kutoka katika shule 10 zilizotembelewa uwiano wa walimu kwa wanafunzi ni mzuri. Kama ilivyo katika wilaya/Halmashauri zingine, uwiano huu unachagizwa na uwepo wa walimu wengi wa masomo ya sanaa kuliko masomo ya sayansi.

Manispaa ya Singida

Mwaka	2015	2016
Shule	Uwiano	Uwiano
Mughanga	1:35	1:40
Unyamikumbi	1:30	1:32
Unyambwa	1:23	1:25
Senge	1:50	1:49
Mandewa	1:32	1:34
Mwankoko	1:24	1:27
Ipembe	1:31	1:35
Mungumaji	1:35	1:40
Kindai	1:52	1:36
Mtamaa	1:20	1:22

Takwimu kutoka katika shule zilizotembelewa zinaonyesha kuwa na viwango tofauti vya uwiano. Shule kama ***Kindai*** na ***Senge*** zikiwa na uwiano mkubwa ukilinganisha na shule ya Unyambwa na unyamikumbi. Kwa miaka ya hivi karibuni uwiano wa walimu na wanafunzi hasa kwa shule za sekondari umekuwa mgumu kupatikana kutokana na kuwepo na upungufu wa walimu wa masomo ya sayansi hivyo kulazimika walimu wa masomo ya sayansi kufundisha vidato vyote wakati walimu wa masomo yasiyo ya sayansi kuwa wengi zaidi hivyo uwiano wao na wanafunzi ni mzuri. ***Mfano; Shule ya Unyamikumbi ina mwalimu mmoja tu wa somo la fizikia,*** *hivyo kulazimika kufundisha vidato vyote.*

Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu

Shule	2015			2016		
	Wanafunzi	Walimu	Uwiano	Wanafunzi	Walimu	Uwiano
Bogwe	699	9	78:1	658	11	59:1
Hwazi	581	48	12:1	520	48	10:1
Nyansha	356	35	10:1	788	35	22:1
Murufiti	236	16	14:1	213	16	13:1
Kigodya	291	18	16:1	286	18	15:1
Kinkati	518	8	64:1	551	8	68:1
Kasange	419	17	24:1	337	17	19:1
Mubondo	174	18	9: 1	185	18	10:1
Nyumbigwa	234	15	15:1	269	15	17:1
Muka	492	9	55:1	481	9	53:1

Uwiano ni mkubwa kwenye baadhi ya shule kama vile ***Mrubona, Kumsenga na Msambala.*** Pia katika miaka hiyo hapakuwa na ongezeko la walimu isipokuwa kwa shule ya Bogwe.

Maoni

Hapakuwa na changamoto kubwa ya namna ya kupata ***uwiano halisi wa Walimu na wanafunzi katika shule za sekondari*** japo kuna takwimu zinaonyesha uwiano kuwa ni mkubwa mzuri kwenye baadhi ya shule. Changamoto iliyopo ni kuwa idadi kubwa ya walimu walioainishwa hapo juu ni wa masomo ya sanaa; Shule nyingi zilizotembelewa zimekutwa na walimu wawili, au Mmoja na hivyo kulazimika kufundisha vidato vyote. Kwa hali hii tusitegemee muujiza katika kufaulisha wanafunzi katika masomo ya sayansi. Pamoja na juhudi zilizopo, jitihada za makusudi zinahitajika kupunguza au kuondoa kabisa tatizo hili la upungufu wa walimu wa masomo ya sayansi.

2.7. Uwiano wa wanafunzi kwa kila chumba cha darasa/Ujazo wa wanafunzi Katika darasa

Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano unakusudia kufikia uwiano wa 40:1 kufikia 2020/21 na 2025/26 kutoka 43:1 kitaifa. Takwimu zifuatazo hapa chini ni kutoka katika shule 10 zilizofanyiwa tafiti ili kuona kama tunapiga hatua kuelekea 2020/21au kuna jitihada zinahitajika ili kufikia lengo hilo.

Manispaa ya Mtwara Mikindani

Jina la Shule	2015											
	Kidato 1			Kidato 2			Kidato 3			Kidato 4		
	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla
Mitengo	25	26	51	19	21	40	33	28	61	19	8	28
Mangamba	14	19	33	11	9	20	29	48	77	26	24	50
Sabasaba	59	64	123	77	71	148	80	76	156	84	89	173
Chuno	48	47	95	45	55	100	54	49	103	71	69	140
Shangani	63	70	133	51	53	104	62	54	116	71	80	151
Umoja	65	68	133	60	45	105	50	48	98	46	52	98
Rahaleo	62	66	128	63	36	99	55	52	107	61	61	122
Naliendele	54	83	137	49	28	77	44	43	87	42	28	70
Sino	56	34	90	61	19	70	45	35	80	41	27	58
Mikindani	21	10	31	19	18	37	29	30	59	21	20	41
Jumla	**467**	**487**	**954**	**455**	**355**	**800**	**481**	**463**	**944**	**482**	**458**	**931**

Jina la Shule	2016											
	Kidato 1			Kidato 2			Kidato 3			Kidato 4		
	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla
Mitengo	60	56	116	28	31	59	13	7	20	33	28	61
Mangamba	52	58	110	12	17	29	13	6	19	27	43	70
Sabasaba	70	61	131	67	75	142	55	65	120	80	76	156
Chuno	45	64	109	55	53	108	38	47	85	53	47	100
Shangani	41	47	88	74	74	148	42	42	84	67	51	118
Umoja	65	66	131	56	75	131	46	28	77	49	47	96
Rahaleo	55	71	126	84	57	141	42	32	74	49	52	101
Naliendele	48	92	140	51	66	117	26	22	48	42	39	81
Sino	54	32	86	67	25	72	49	36	84	40	29	59
Mikindani	64	79	143	21	15	36	14	9	23	27	29	56
Jumla	**554**	**626**	**1180**	**515**	**488**	**983**	**338**	**294**	**634**	**467**	**441**	**898**

Takwimu hapa hapo juu zinaonyesha idadi ya wanafunzi kwa kila chumba cha darasa kwa shule 10 za Sekondari Manispaa ya Mtwara Mikindani. Utafiti unaonyesha hakuna uwiano tarajiwa wa idadi ya wanafunzi kwa kila chumba cha darasa.

Kwa mujibu wa sera ya elimu na mpango wa Maendeleo wa miaka 5 mwaka 2016/2017 – 2020/2021 idadi ya wanafunzi kwa kila chumba cha darasa/mkondo ni 40:1 lakini hali halisi ujazo wa wanafunzi katika darasa ni mkubwa; mwaka 2015 kwa hiyo mfano ukichukulia shule ya Naliendele ina wanafunzi 137 lakini ina mikondo 2 tu ambayo ni sawa na wanafunzi 69 kwa mkondo hivyo kuna ongezeko la wanafunzi 29 kila mkondo**.**

Pia shule ya Sabasaba kwa mwaka 2015 kidato cha nne kulikuwa na wanafunzi 173 ikiwa ni wastani wa wanafunzi 87 kwa chumba cha darasa. Pia shule ya Shangani mwaka 2016 kidato cha pili wanafunzi 148 kwa wastani wa 74 kila chumba.

Mlundikano wa wanafunzi darasani hupunguza ufanisi wa walimu katika ufundishaji pia wanafunzi kukosa usikivu na ukosefu wa hewa ya kutosha kwenye chumba cha darasa hali inayoweza kusababisha magonjwa mbalimbali ikiwemo ya mlipuko, haya na mengineyo huchangia kushusha kiwango cha elimu mfano ni matokeo ya kidato cha nne mwaka 2016 shule za Manispaa ya Mtwara Mikindani zimepata matokeo mabaya.

Manispaa ya Temeke

	2015			2016		
Shule	**Wanafunzi**	**Vyumba**	**Uwiano**	**Wanafunzi**	**Vyumba**	**Uwiano**
Pendamoyo	1402	12	1:117	1350	12	1:113
Mibulani	1331	16	1:83	1340	16	1:84
Wailes	1682	14	1:120	1543	16	1:96
Saku	1292	13	1:108	1629	13	1:125
Malela	901	12	1:75	943	12	1:79
Changanyikeni	825	13	1:63	932	14	1:67
Mikwambe	957	14	1:68	897	16	1:56
Toangoma	1051	18	1:58	1207	18	1:67
Tandika	1752	16	1:110	1791	16	1:112
Lumo	1222	12	1:102	1289	13	1:99

Takwimu: Elimu Manispaa ya Temeke

Mwaka	2015	2016
Kidato cha Kwanza	1:109	1:145
Kidato cha Pili	1:100	1:113
Kidato cha tatu	1:78	1:110
Kidato cha nne	1:75	1:94

Kutoka katika shule 10 zilizotembelewa uwiano wa wanafunzi kwa kila chumba cha darasa ni kubwa ukilinganisha na vyumba vya madarasa vilivyopo shule za sekondari. Darasa lenye uwiano wa 1:75, 1:110, 1:56, 1:120 ni ngumu mwalimu kulimudu darasa hilo na wanafunzi kuelewa nini mwalimu anafundisha. Lakini pia uwiano wa Kimanispaa bado ni mkubwa sana. Sera na Mpango wa Maendeleo una nia ya kufikisha 40:1 kufikia 2020/2021. Hakika bado kuna kazi kubwa inayotakiwa kufanyika ili kuboresha mazingira hayo.

Manispaa ya Singida

Na.	SHULE	KIDATO	2015			2016		
			Wav	Was	Jumla	Wav	Was	Jumla
	Mughanga	Kidato 1	62	66	128	72	88	160
		Kidato 2	63	69	132	58	66	124
		Kidato 3	73	94	167	63	69	132
		Kidato 4	69	76	145	73	96	169
	Unyamikumbi	Kidato 1	21	36	57	20	20	40
		Kidato 2	09	23	32	10	19	29
		Kidato 3	22	32	54	11	23	34
		Kidato 4	13	22	35	11	18	29
	Unyambwa	Kidato 1	21	23	44	24	23	47
		Kidato 2	14	12	26	21	19	40
		Kidato 3	13	24	37	11	10	21
		Kidato 4	12	15	27	09	20	29
	Senge	Kidato 1	52	76	138	69	78	147
		Kidato 2	50	57	107	58	79	137
		Kidato 3	69	68	137	58	79	137
		Kidato 4	94	76	170	69	68	137
	Mandewa	Kidato 1	44	60	104	44	81	125
		Kidato 2	43	54	97	51	65	116
		Kidato 3	45	54	99	30	41	71
		Kidato 4	45	39	84	36	47	83
	Mwankoko	Kidato 1	13	24	37	16	16	32
		Kidato 2	33	22	55	15	22	37
		Kidato 3	25	28	53	22	20	42
		Kidato 4	20	15	35	22	24	46
	Ipembe	Kidato 1	44	53	97	59	66	125
		Kidato 2	49	41	90	48	46	94
		Kidato 3	34	59	93	40	38	78
		Kidato 4	46	61	107	34	56	90

	Mungumaji	Kidato 1	48	38	86	39	56	95
		Kidato 2	36	27	63	37	37	74
		Kidato 3	45	47	92	22	26	48
		Kidato 4	46	37	83	40	45	85
	Kindai	Kidato 1	40	40	80	71	67	138
		Kidato 2	43	69	112	35	38	73
		Kidato 3	51	65	126	40	59	99
		Kidato 4	43	56	99	47	59	106
	Mtamaa	Kidato 1	15	15	30	29	43	73
		Kidato 2	28	18	46	17	17	34
		Kidato 3	14	11	25	19	14	33
		Kidato 4	16	13	29	14	12	26

Takwimu: Elimu Manispaa ya Singida

Mwaka	2015	2016
Kidato cha 1	1:35	1:44
Kidato cha 2	1:34	1:35
Kidato cha 3	1:38	1:31
Kidato cha 4	1:37	1:21

Taarifa ya idara ya elimu sekondari 2015-2016 inaonesha kuwa uwiano wa vyumba vya madarasa na wanafunzi ni 1:30 kwa mwaka 2015 na 1:31 kwa mwaka 2016. Ingawa utafiti unaonesha kuwa shule nyingi za sekondari zina uwiano mzuri wa vyumba vya madarasa na wanafunzi ingawa pia kuna uhaba wa vyumba vya madarasa kwa baadhi ya shule. Jedwali hapo juu linaonyesha idadi ya wanafunzi kwa kidato (ingawa sio wote wanasomea chumba kimoja cha darasa).

Kwa kuzingatia takwimu kama zilivyoainishwa hapa juu, ni dhahili kuwa bado kuna hitaji kubwa la vyumba vya madarasa ili kuweza kukidhi ongezeko la idadi ya wanafunzi hasa kutokana na mpango wa hivi sasa wa elimu bila malipo. Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (5) katika utekelezaji wake unalenga kufikia uwiano wa 40:1 kwa mwaka 2020/21 na 2025/26 kutoka 43:1. Mlundikano wa wanafunzi wengi darasani hautoi fursa nzuri kwa wanafunzi kujifunza sawasawa lakini pia kuwa ni changamoto kwa walimu husika.

❖ HALI HALISI KATIKA PICHA

Uwiano wa wanafunzi kwa kila chumba cha darasa

Picha 1: Toangoma sekondari; Temeke

Picha 2: Wailes sekondari; Temeke

Picha 3: Nyansha sekondari: Kasulu

Picha 4: Bogwe sekondari: Kasulu

2.8. Uwiano wa Idadi ya wanafunzi kwa matundu ya vyoo katika Halmashauri

Halmashauri	2015						2016					
	Me	Idadi	Uwiano	Ke	Idadi	Uwiano	Me	Idadi	Uwiano	Ke	Idadi	Uwiano
Mtwara Manispaa	2621	89	1:29	2837	89	1:32	2582	89	1:29	3094	89	1:35
Morogoro Manispaa	6978	155	1:45	8633	259	1:33	7074	152	1:47	8782	283	1:31
Ilemela	8267	130	1:64	8667	129	1:67	8487	134	1:63	8352	135	1:62
Temeke Manispaa	21074	130	1:162	22289	156	1:142	20079	182	1:110	22645	208	1:108
Singida Manispaa	3152	128	1:25	3405	128	1:27	3625	141	1:26	3135	141	1:22
Urambo	3753	72	1:52	3292	72	1:45	2294	72	1:31	2152	72	1:39
Mbeya vijijini	4809	211	1:22	6173	236	1:26	4532	223	1:20	5861	257	1:22

Jedwali Na 7: Uwiano wa Idadi ya wanafunzi kwa matundu ya vyoo katika Halmashauri
Takwimu hapo juu ni kutoka Halmashauri/wilaya saba (7) kati ya kumi (10) zilizofanyiwa utafiti ili kuona hali ya uwiano wa vyoo na idadi ya wanafunzi katika ngazi ya Halmashauri. Hali ya miundombinu ya vyoo imekuwa ikichangia sana wanafunzi kukatiza masomo yao pale miundombinu ya vyoo ***inapokuwa michache, michakavu au kutokuwepo kabisa***, hasa kwa watoto wa kike wanapokuwa katika siku zao za mwezi (hedhi).

Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano umekusudia kufikia uwiano wa 20:1 kufikia mwaka 2021 na 2025/26 kitaifa. Lakini kwa taarifa kutoka ngazi ya Halmashauri kama zinavyoonekana hapo juu inaonyesha kuwa bado kuna kazi kubwa ya kufanyika ili kufikia lengo.

❖ UWIANO WA IDADI YA WANAFUNZI KWA MATUNDU YA VYOO KUTOKA KATIKA BAADHI YA SHULE 10 ZILIZOTEMBELEWA KATIKA HALMASHAURI HUSIKA

Manispaa yaTemeke

Jina la Shule	2015						2016					
	Wanafunzi		Matundu ya vyoo		uwiano		Wanafunzi		Matundu ya vyoo		Uwiano	
	Me	Ke	Me	Ke	Me	Ke	Me	Ke	Me	Ke	Me	Ke
Pendamoyo	723	679	04	04	1:181	1:170	655	695	04	04	1:164	1:174
Miburani	649	682	08	08	1:81	1:85	638	702	08	08	1:80	1:88
Wailes	844	838	04	05	1:211	1:168	689	854	07	09	1:98	1:95
Saku	589	703	05	05	1:118	1:141	842	787	07	08	1:120	1:98
Malela	362	539	04	05	1:91	1:108	405	538	04	05	1:101	1:108
Changanyikeni	325	500	04	06	1:81	1:83	330	602	04	06	1:83	1:100
Mikwambe	425	532	05	05	1:85	1:106	315	582	05	05	1:63	1:116
Toangoma	565	486	09	12	1:63	1:41	506	701	09	12	1:56	1:58
Tandika	819	933	05	05	1:164	1:187	810	981	05	05	1:162	1:196
Lumo	571	651	05	05	1:114	1:130	603	686	05	05	1:121	1:137

Utafiti 2017

Takwimu hapo juu kutoka katika shule 10 zilizotembelewa zinaonyesha uwiano wa wanafunzi na matundu ya vyoo ni mkubwa sana. Hii inamaanisha kwamba matundu ya vyoo ni machache sana ukilinganisha na idadi ya wanafunzi. *Kama hatua za makusudi hazitachukuliwa na mamlaka husika, lengo la kufikia uwiano wa 20:1 kufikia mwaka 2020/21 na 2025/26 halitafikiwa.*

Hali halisi ya vyoo vinavyotumika katika picha: Temeke, Dar es salaam

Picha 5: Tandika sekondari

Picha 6: Changanyikeni sekondari

Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto

	Shule	wav	vyoo	Uwiano	was	vyoo	Uwiano
1	Balozi Mshangama	62	3	1:21	119	3	1:40
2	Gare	61	8	1:8	131	8	1:16
3	Kisaba	148	6	1:25	243	10	1:24
4	Kitala	84	6	1:14	96	6	1:16
5	Masange	125	7	1:18	267	7	1:38
6	Ngazi	95	5	1:19	119	5	1:24
7	Ngulwi	83	4	1:21	92	4	1:23
8	Prince Claus	74	2	1:37	96	2	1:48
9	Shita	91	5	1:18	183	5	1:37
10	Ubiri	190	5	1:38	311	5	1:62

Lengo la Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ni 20:1 kufikia 2020/21 na 2025/26. Kwa takwimu tajwa hapo juu, muelekeo ni mzuri kufikia lengo hilo.

Hali halisi ya vyoo vinavyotumika Katika Picha: Lushoto (Baadhi ya shule)

Picha 7: choo wavulana, Gare sekondari

Picha 8: choo wasichana Balozi Mshangama sekondari

Halmashauri ya Wilaya Kasulu

shule	Wanafunzi 2015		Jumla	Matundu Ya vyoo		Uwiano	Uwiano	Wanafunzi 2016		Jumla	Matundu Ya vyoo		Uwiano	Uwiano
	Me	Ke		Me	Ke	Me 2015	Ke 2015	Me	Ke		Me	Ke	Me 2016	Ke 2016
Bogwe	339	360	699	5	5	1:68.	1:72	283	375	658	5	5	1:56	1:75
Hwazi	302	279	581	4	4	1:76	1:69	284	286	570	4	4	1:71	1:72
Nyansha	271	225	496	3	3	1:90.	1:75	271	219	490	3	3	1:90	1:73
Murufiti	160	75	235	5	6	1:32	1:12	218	44	262	5	6	1:43	1:7
Kigodya	114	63	177	3	3	1:38	1:21	111	64	175	4	3	1:27	1:21
Mubondo	100	74	174	3	6	1:33	1:12	125	60	185	3	6	1:41	1:10
Kinkati	301	217	518	8	6	1:37	1:36	324	227	554	8	6	1:40	1:37
Muka	274	197	471	11	14	1:24	1:14	271	173	444	11	12	1:24	1:14
Kasange	235	182	417	8	10	1:29	1:18	211	136	347	12	14	1:17	1:9
Nyumbigwa	153	82	235	4	6	1:38	1:13	172	97	269	4	6	1:43	1:16

Hali halisi ya vyoo vinavyotumika katika Picha: Kasulu

Picha 9&10: Mbondo sekondari

Picha 11&12: Mrufi sekondari

Manispaa ya Mtwara Mikindani

Jina la Shule	2016					Uwiano	
	Idadi		Jumla	Matundu ya vyoo		me	ke
	me	ke		me	ke		
Mitengo	130	132	262	4	8	33:1	17:1
Mangamba	104	124	228	4	6	26:1	21:1
Sabasaba	272	277	549	16	16	17:1	17:1
Chuno	191	211	402	4	4	48:1	53:1
Shangani	224	214	438	4	4	56:1	54:1
Umoja	216	216	432	4	4	54:1	54:1
Rahaleo	230	212	442	6	6	38:1	35:1
Naliendele	167	219	386	6	8	28:1	27:1
Sino	211	278	489	6	10	35:1	28:1
Mikindani	115	126	241	4	4	29:1	32:1

Picha 13 na 14: Choo wavulana, Sabasaba sekondari; Mtwara Mkindani

Kwa kuzingatia takwimu zilizotolewa hapo juu pamoja na picha halisi ya mazingira ya vyoo vinavyotumiwa na wanafunzi katika maeneo tofauti. Ni dhahili kuna kazi ya ziada inahitajika kufanyika ili kuweza kufikia lengo la uwiano wa 20:1 ifikapo mwaka 2020/21 na 2025/26 ili kuwa na mazingira bora ya wanafunzi kujifunzia.

2.9. Shule zenye umeme

Katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2020/21, serikali imejiwekea lengo la kuwa na umeme katika shule za sekondari kwa asilimia 85% kutoka asilimia 77.3% mwaka 2014/15. TCDD inalenga kupima maendeleo ya mpango huu katika mwaka wa pili wa utekelezaji wa mpango huo, ili kuweza kuishauri serikali ili mpango huo uweze kufanikiwa kwa wakati ili kuwa na mazingira bora ya utolewaji wa elimu.

Jedwali Na 8

	Shule Zenye Umeme Kati ya 10 Zilizotembelewa	
Wilaya	**2015**	**2016**
Mtwara Manispaa	Shule 8 zina umeme	Shule 8 zina umeme
Morogoro Manispaa	Shule zote 10 zina umeme	Shule zote 10 zina umeme
Temeke	Shule zote 10 zina umeme	Shule zote 10 zina umeme
Singida Manispaa	Shule 4 zina umeme	Shule 4 zina umeme
Kasulu	Shule 1 ina umeme	Shule 1 ina umeme
Mbeya Vijijini	Shule 5 zina umee	Shule 5 zina umeme
Ilemela	Shule zote 10 zina umeme	Shule zote 10 zina umeme
Arumeru Magharibi	Shule 6 zina umeme	Shule 6 zina umeme
Urambo	HT	HT
Lushoto	HT	HT

HALI YA MIUNDOMBINU MINGINE

Picha 15 (Chini): Maabara

Kabuhoro Sekondari

Picha 16

Nyamanoro Sekondari

Picha 17: Shule ya Sekondari Pasiansi

Picha 18 Shule ya Sekondari Nyumbigwa

Majengo ya maabara yakiwa hayajakamilika kutoka katika shule ya Kabuhoro, Nyamanoro na Pasiansi toka mwaka 2005, Manispaa ya Ilemela. Jengo la maabara shule ya Nyumbigwa (juu kulia) likiwa limeezuliwa na upepo na kutelekezwa, Kasulu.

Jiko

Picha 19: Hali ya Jiko la kupikia chakula cha wanafunzi na bwalo la chakula, shule ya Malela, Temeke.

Picha 20: Hili ni darasa linalotumika na wanafunzi wa kidato cha tatu (3) katika Shule ya Uwanja wa Taifa, Morogoro Manispaa.

Picha 21

Hivi ni baadhi ya vyumba vya madarasa vilivyokuwa vimeanza kujengwa kwa nguvu ya wananchi. Baada tu ya mpango mzuri wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutangaza Mpango wa Elimu bila malipo majengo mengi yametelekezwa bila kuendelezwa katika **shule ya sekondari Hwazi** iliyoko Halmashauri ya mji Kasulu.

Picha 22

Picha ya baadhi ya walimu wa **shule ya Sekondari Hwazi** wakifanyia kazi zao chini ya mti walivyokutwa na mfuatiliaji kutokana na uhaba wa ofisi. Pia Mwalimu Mkuu akiwa katika ofisi iliyozibwa na bati.

MAONI YA WADAU
BODI ZA SHULE, WALIMU, WAZAZI, KAMATI ZA MAENDELEO YA KATA NA WANAFUNZI

Changamoto za upatikanaji wa elimu

- Uhaba wa walimu wa sayansi
- Uzembe na utoro wa wanafunzi
- Walimu wachache ambao hawakidhi mahitaji
- Maabara nyingi kutokufanya kazi
- Mila na desturi potofu kutoka kwa jamii
- Ugumu wa lugha inayotumika kufundishia kiingereza (english)
- Wazazi kutokuwajibika kikamilifu katika kuwasimamia na kuwafuatilia watoto wao
- Kukosekana kwa chakula cha mchana Mashuleni
- Ukosefu wa vifaa vya kufundishia kama vile vifaa vya maabara na vitabu
- Wanafunzi kuwa na mahusiano ya kimapenzi na kuathiri masomo yao
- Mimba kwa watoto wa kike
- Ukosefu wa miundombinu hasa ya vyoo ambayo ni rafiki kwa wanafunzi wa kike hasa kipindi wanapokuwa katika kipindi cha hedhi hivyo kushindwa kuhudhuria masomo yao vizuri
- Ukosefu wa mabweni kwa wasichana katika shule nyingi hivyo kusababisha watembee umbali mrefu kwenda shule wakati wengine wakiamua kupanga hosteli mitaani ambako hukumbana na vishawishi vingi na mwisho wa siku kukatishwa masomo baada ya kupata ujauzito.
- Jamii kuwa na uelewa mdogo juu ya umuhimu wa elimu kwa watoto wa kike na muda mwingine kuchelewa kuwaandikisha shuleni.
- Baadhi ya wanafunzi wa kike huacha shule na kwenda kuajiriwa kufanya kazi za ndani (house girl) hivyo kukatisha masomo yao.

Nini kifanyike Kuboresha Upatikanaji wa Elimu

- Serikali na wadau wengine wa elimu waweke mikakati madhubuti ya kuajiri walimu wengi wa sayansi na hisabati ili kuondoa uhaba uliopo sasa.
- Serikali ni vyema ikatenga bajeti ya kutosha kwa ajili shule za sekondari ili kuboresha mazingira ya kujifunzia kwa wanafunzi kama vile kuongeza madarasa kulingana na idadi ya wanafunzi.
- Serikali inapaswa kuangalia maslahi ya walimu ili kuwapa motisha na hivyo kutoa elimu bora.
- Uongozi wa kisiasa katika Kata husika uendelee kuielimisha jamii kuhusu umuhimu wa elimu kwa watoto wao ili wachangie maendeleo ya elimu ya sekondari.
- Uwepo utaratibu wa utoaji chakula katika shule za sekondari ili kuwezesha wanafunzi kusoma vizuri kwani wengi wanatoka katika familia zenye hali duni na wengine kushindwa kurudi nyumbani kupata chakula kutokana na umbali.
- Maabara zikamilishwe kwa wakati na kupatiwa vifaa vyake ili kuwezesha wanafunzi kujifunza kwa vitendo na sio kwa nadharia tu, hii itachangia kuongeza ufaulu katika masomo ya sayansi.
- Serikali na wadau wa sekta ya elimu washirikiane kuhakikisha upatikanaji wa vitabu vya kutosha unakuwepo kwa shule zote ili kuwapa fursa walimu kufundisha vizuri na wanafunzi kujisomea.
- Serikali ijenge nyumba za watumishi na mabweni kwa ajili ya wanafunzi waishio mbali na shule hizo ili kupunguza utoro na vishawishi vinavyoweza kuwapata wanafunzi hasa wakike
- Serikali kwa kushirikiana na wadau wa elimu wajenge mabweni kwa ajili ya wanafunzi wa kike ili waweze kupata muda mwingi wa kujisomea na pia kuwaepusha na vishawishi mitaani
- Kuboresha miundombinu ya vyoo na hasa chumba maalumu kwaajili ya kujistiri kwa wale wanaokuwa katika hedhi ili kutoathiri mahudhurio yao darasani.

SURA YA TATU

UFUATILIAJI WA MRADI WA 2014 – 2016 (BACKSTOPPING)

3.0. UTANGULIZI

Sehemu hii inahusisha taarifa za mradi uliotekelezwa na TCDD kipindi cha mwaka 2014 hadi 2016 katika mradi wa kufuatilia umaskini na unawajibikaji kupitia Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa 2016/17 -2020/21 katika sekta za elimu. Katika hatua hii taarifa zinazokuja zinajaribu kuonyesha matokeo ambayo mradi imeyaleta baada ya utekelezaji wa mradi kuwa ulishafanyika kwa kipindi kilichotajwa hapo juu.

3.1. Sekta ya elimu

Ufuatiliaji huu ulifanyika mwaka 2017 kwa kujikita katika viashilia vya elimu vilivyoorodheshwa katika mpango wa maendeleo kwa lengo la kujipima kuona kama malengo yaliyowekwa na serikali kufikia mwaka 2020/21 yanatekelezeka ama hayatekelezeki.

3.2. Halmashauri zilizohusika

Wilaya	Taasisi iliyohusika
Bunda	FOUNDATION HELP
Rungwe	ELIMISHA
Magu	SDI
Mufindi	TDGPA
Kigoma Vijijini	KIUNGONET
Mkuranga	TARUCODEFU
Newala	FAWOPA
Lindi Manispaa	LINGONET
Kishapu	TAHEA

Utafiti 2017

MATOKEO YA UFUATILIAJI

3.3. Jumla ya wanafunzi walioandikishwa kidato cha kwanza 2015 na 2016

Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (5) Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (5) unakusudia kufikisha asilimia 50% ya uandikishaji wa wanafunzi wa kidato cha kwanza kufikia mwaka 2020/21 na asilimia 90% kufikia 2025/26. Takwimu hapa chini zinaonyesha hali ya uandikishaji wa wanafunzi katika kila shule zilizotembelewa na ngazi ya Halmashauri.

Katika ngazi ya Shule

Wilaya		2015			2016		
	Idadi ya Shule	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla
Rungwe	8	965	968	1933	950	1030	1980
Newala	6	153	196	349	255	253	508
Bunda	10	776	453	1229	1005	754	1759
Mkuranga	10	379	548	937	594	463	1057
Magu	10	869	763	1632	984	837	1821
Kishapu	10	463	539	1002	604	614	1218
Mufindi	10	753	743	1496	775	990	1765



KATIKA NGAZI YA HALMASHAURI

Rungwe

Mwaka	2015			2016		
Jinsi	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla
Kidato cha 1	1,597	1879	3,476	1593	1992	585

Kigoma vijijini

Mwaka	2015			2016		
Jinsi	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla
Kidato cha 1	483	271	754	585	385	970

Lindi Manispaa

Mwaka	2015			2016		
Jinsi	Me		Jumla	Me	Ke	Jumla
Kidato cha 1	360	331	691	455	515	970

Mkuranga

Mwaka	2015			2016		
Jinsi	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla
Kidato cha 1	994	1185	2179	962	1117	2099

Kishapu

Mwaka	2015			2016		
Jinsi	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla
Kidato cha 1	1,312	1,233	2,545	1,593	1,526	3,119

Takwimu kutoka ngazi ya Elimu Wilaya na Elimu katika wilaya zote zinaonyesha kuongezeka kwa uandikishaji wa wanafunzi kwa miaka yote miwili yaani mwaka 2015 na mwaka 2016. Mwelekeo huu unaonyesha kuwa lengo la kufikia asilimia 50% katika uandikishaji wa wanafunzi wa kidato cha kwanza linaweza kufikiwa kufikia mwaka 2020/21, pia hali ya uandikishaji wa wanafunzi wa jinsi ya kike umeonekana kuimarika na kuonekana kuwa ni mkubwa kwenye baadhi ya maeneo kuliko wanafunzi wa jinsi ya kiume kama takwimu zionekanavyo.

3.4. Wanafunzi waliochaguliwa na hawakuripoti shuleni

Katika ngazi ya Shule

Kishapu

Mwaka	2015			2016		
Shule	**Me**	**Ke**	**Jumla**	**Me**	**Ke**	**Jumla**
Ufundi Mwadui	3	6	9	0	0	0
Kishapu	8	8	16	7	4	11
Maganzo	1	7	8	5	5	10
Mwigumbi	11	13	24	0	2	2
Mangu	6	1	7	5	3	8
Mwataga	0	1	1	0	0	0
Mwamaduli	2	1	3	3	2	5
Uchunga	2	4	6	0	0	0
Idukilo	14	22	36	3	0	3
Bunambiyu	0	0	0	1	0	1
Jumla	**47**	**63**	**110**	**24**	**16**	**40**

Manispaa ya Lindi

Shule /Mwaka	2015			2016		
Jinsi	**Me**	**Ke**	**Jumla**	**Me**	**Ke**	**Jumla**
Chikonji	0	0	0	0	0	0
Kineng'ene	5	2	7	7	7	14
Nga'pa	4	4	8	1	1	2
Ngongo	0	0	0	1	0	0
Mingoyo	0	0	0	0	0	0
Lindi	0	0	0	0	0	0
Mkonge	13	10	23	3	9	12
Angaza	0	0	0	0	0	0
Jumla	**22**	**16**	**38**	**12**	**17**	**28**

Bunda

Shule/Mwaka	2015			2016		
	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla
Nyiendo	7	7	14	15	9	24
Sizaki	4	5	9	4	3	7
Kabasa	18	17	35	24	16	40
Wariku	13	1	14	5	5	10
Mihingo	2	0	2	1	1	2
Mekomarilo	8	3	11	2	4	6
Chamriho	10	10	20	6	10	16
Guta	12	3	15	13	18	31
Muranda	13	7	20	11	5	16
Chitengule	18	4	22	12	11	23
Jumla	**105**	**57**	**162**	**93**	**82**	**175**

Mufindi

Shule/Mwaka	2015			2016		
	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla
Makalala	1	5	6	2	3	5
Igowole	0	0	0	0	0	0
Mninga	0	0	0	0	0	0
Kasanga	20	24	44	13	12	25
Ihongore	2	4	6	1	3	4
J J Mungai	0	0	0	0	0	0
Mnyigumba	7	2	9	4	2	6
Changarawe	5	3	8	0	8	8
Luganga	67	18	85	7	25	32
Kinyanambo	12	5	17	10	14	24
Jumla	**114**	**61**	**175**	**37**	**67**	**104**

Magu

Shule/Mwaka	2016			2016		
	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla
Lubugu	8	10	18	3	4	7
Magu	119	115	234	117	114	231
Kinago	-	-	-	4	3	7
Itumbili	7	9	16	8	20	28
Sukuma	18	21	39	7	2	9
Ng'haya	41	41	82	6	9	15
Mugini	-	-	-	-	-	-
Kahangara	6	12	18	5	10	15
Kandawe	35	21	56	-	-	-
Ng'wamabanza	1	4	5	2	1	3
Jumla	**235**	**233**	**468**	**152**	**163**	**315**

Ngazi ya Wilaya/Halmashauri

Kishapu

Mwaka	2015			2016		
Jinsi	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla
Kidato cha 1	115	342	457	53	112	165

Rungwe

Mwaka	2015			2016		
Jinsi	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla
Kidato cha 1	186	184	370	121	133	254

Kigoma Vijijini

Mwaka	2015			2016		
Jinsi	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla
Kidato cha 1	70	55	125	53	45	98

Mkuranga

Mwaka	2015			2016		
Jinsi	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla
Kidato cha 1	112	193	305	122	151	273

Mufindi

Mwaka	2015			2016		
Jinsi	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla
Kidato cha 1	62	74	136	76	111	187

Takwimu za wanafunzi ambao hawaripoti baada ya kuwa wamechaguliwa na kujiunga na kidato cha kwanza imezidi kuongezeka mwaka hadi mwaka. Hali hii inapelekea tatizo hili kuwa sugu na kuonekana ni la kawaida kwenye baadhi ya Halmashauri.

Kuna sababu mbalimbali zimetajwa kutoka katika shule ambazo zilitembelewa zinazodaiwa kusababisha wanafunzi kutoripoti shuleni mara wanapochaguliwa nazo ni kama zilivyoainishwa:

- Walijiunga katika shule za watu binafsi (Private)
- Utoro
- Mwamko mdogo wa elimu
- Hali ngumu ya Uchumi kwa baadhi ya wazazi
- Shughuli za Kilimo, Ufugaji (kuchunga), Uvuvi, Machimbo madogo (Migodini) na Uwindaji. Pia watoto kuacha shule na kujikita katika biashara ndogondogo
- Kuhama

Mfano: Katika Halmashauri ya Rungwe mwaka 2016 takribani wanafunzi 81 walikataa kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza na wengine kutoroka mara baada ya kuwa wameshajiunga.

3.5. Idadi ya wanafunzi waliofanya mtihani wa kidato cha nne na waliofaulu

Serikali kupitia Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka 5 ni kuhakikisha inafikia ufaulu kwa asilimia 80% kufikia mwaka 2020/21 na 90% kufikia mwaka 2025/26. Taarifa hii inaonyesha mwenendo usioridhisha juu ya ufaulu wa wanafunzi katika mtihani wa kidato cha nne kwa mwaka 2015 na 2016 hivyo kutia shaka lengo kufikiwa: Takwimu hapa chini zinaonyesha:-

Bunda	**2015**		**2016 - JUMLA**	
Watahiniwa	1032	65%	968	64%
Waliofaulu	554	35%	556	36%

2015	**Me**		**Ke**	
Watahiniwa	599	61%	433	72%
Waliofaulu	385	39%	169	28%

2016	**Me**		**Ke**	
Watahiniwa	563	59%	405	71%
Waliofaulu	391	41%	165	29%

Kigoma vijijini

Mwaka	**2015**			**2016**		
Jinsi	**Me**	**Ke**	**Jumla**	**Me**	**Ke**	**Jumla**
Watahiniwa	489	256	745	281	164	445
Waliofaulu	320	128	448	226	85	311

Manispaa ya Lindi

Waliofanya mtihani

Shule	2015			2016		
Jinsi	**Me**	**Ke**	**Jumla**	**Me**	**Ke**	**Jumla**
Chikonji	16	6	22	12	14	26
Kineng'ene	101	72	173	80	68	148
Nga'pa	40	30	70	44	28	72
Ngongo	32	33	65	16	15	31
Mingoyo	17	14	31	23	25	48
Lindi	36	32	68	53	28	81
Mkonge	90	75	165	70	87	157
Angaza	40	42	82	44	39	83
Jumla	**372**	**304**	**676**	**342**	**304**	646

Waliofaulu

Shule	2015			2016		
Jinsi	**Me**	**Ke**	**Jumla**	**Me**	**Ke**	**Jumla**
Chikonji	10	4	14	4	8	12
Lindi	79	36	105	60	55	115
Ngongo	30	11	41	27	14	41
Kineng'ene	29	30	59	16	15	31
Nga'pa	15	9	24	16	12	28
Mingoyo	33	25	58	37	16	53
Mkonge	48	35	83	30	47	77
Angaza	23	18	31	31	20	51
Jumla	**273**	**168**	**415**	**221**	**187**	**408**

Magu

Waliofanya mtihani

Shule	2015			2016		
Jinsi	**Me**	**Ke**	**Jumla**	**Me**	**Ke**	**Jumla**
Lubugu	52	44	96	52	38	90
Magu	126	127	253	142	105	247
Kinago	85	72	157	100	78	178
Itumbili	82	84	166	75	52	127
Sukuma	52	26	78	50	46	96
Ng'haya	63	35	98	53	33	86
Mugini	-	-	-	8	7	15
Kahangara	59	46	105	54	38	92
Kandawe	89	71	160	66	45	11
Ng'wamabanza	28	33	61	21	16	37
Jumla	**636**	**538**	**1174**	**621**	**458**	**1079**

Waliofaulu

Shule	2015			2016		
	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla
Lubugu	42	13	55	42	27	69
Magu	73	92	165	98	65	163
Kinago	63	42	105	88	55	143
Itumbili	58	29	87	47	16	63
Sukuma	44	8	52	45	14	59
Ng'haya	40	23	63	37	18	55
Mugini	-	-	-	8	7	15
Kahangara	43	13	56	38	14	52
Kandawe	46	24	70	42	14	56
Ng'wamabanza	17	23	40	16	12	28
Jumla	**426**	**267**	**693**	**461**	**242**	**703**

Mufindi

Waliofanya mtihani

Wilaya / Halmashauri	Shule	2015			2016		
		Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla
Mufindi	Mkalala	22	48	70	26	44	70
Mufindi	Igowole	79	132	211	62	72	134
Mufindi	Mninga	19	43	62	16	27	43
Mufindi	Kasanga	31	42	73	17	25	42
Mafinga Mji	Ihongore	66	64	130	36	35	71
Mafinga Mji	J J Mungai	120	124	244	79	88	167
Mafinga Mji	Mnyigumba	23	27	50	13	13	26
Mafinga Mji	Changarawe	91	81	172	67	40	107
Mafinga Mji	Luganga	43	48	91	44	36	80
Mafinga Mji	Kinyanambo	74	80	154	42	58	100
Jumla		**568**	**689**	**1257**	**402**	**438**	**840**

Waliofaulu

Wilaya / Halmashauri	Shule	2015			2016		
		Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla
Mufindi	Mkalala	13	26	39	13	25	38
Mufindi	Igowole	34	73	107	46	57	103
Mufindi	Mninga	11	20	31	11	22	33
Mufindi	Kasanga	27	28	55	16	16	32
Mafinga Mji	Ihongore	42	44	86	34	29	63
Mafinga Mji	J J Mungai	91	87	178	76	84	160
Mafinga Mji	Mnyigumba	16	18	34	12	12	24
Mafinga Mji	Changarawe	67	55	122	63	34	97
Mafinga Mji	Luganga	38	40	78	33	31	64
Mafinga Mji	Kinyanambo	51	42	93	34	39	73
Jumla		**390**	**433**	**823**	**338**	**349**	**687**

Mkuranga

Jina la shule	Waliotahiniwa						Waliofaulu					
	2015			2016			2015			2016		
	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla
Mkugilo	14	22		16	32	48	07	08	15	06	02	08
Mwalusembe	29	18		26	22	48	28	11	39	19	13	32
Mkamba	28	22		39	31	70	15	12	27	16	17	33
Tengelea	20	16		18	18	36	09	09	18	10	05	15
Tambani	21	18		08	13	21	16	09	25	08	12	20
Dundani	31	37		29	32	61	22	20	42	12	11	23
Kisiju pwani	15	11		08	14	22	09	05	14	07	05	12
Kiparang'anda	20	23		36	37	73	14	10	24	21	18	39
Vikindu	53	45		101	84	185	35	19	54	32	26	58
Mwinyi	91	73		65	71	136	33	16	49	43	35	78

Kwa mujibu wa takwimu hapo juu, zinaonyesha hakuna uwiano mzuri kati ya wanafunzi wanaotahiniwa na wanafunzi wanaofaulu. Idadi ya wanafunzi wanaofualu kwa ufaulu wa daraja I, II, III na IV ni ndogo sana ukilinganisha na idadi ya jumla ya watahiniwa kwa mwaka husika. Hii inamaanisha kuwa hali ya ufaulu bado ni ndogo sana. Pia kutoka katika idadi hiyo ndogo ya wanafunzi wanaofaulu sio wote wana vigezo vya kujiunga na kidato cha 5 hasa kwa wenye ufaulu wa daraja la nne (IV).

3.6. Uwiano wa Idadi ya walimu na wanafunzi

Katika Mpango huu wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (5), serikali imekusudia kufikia uwiano wa 20:1 yaani wanafunzi ishirini kwa mwalimu mmoja. Ufuatiliaji ukajikita katika kutafuta taarifa na kuona hali ikoje hivi sasa katika shule zetu wakati utekelezaji ukiendelea kufikia mwaka 2020/21 na 2025/26.

Newala

	2015			2016		
Darasa	Wanafunzi	Walimu	Jumla	Wanafunzi	Walimu	Jumla
Kidato cha 1	379	53	7:1	526	43	12:1
Kidato cha 2	293	52	5:1	422	56	7:1
Kidato cha 3	239	50	4:1	163	52	3:1
Kidato cha 4	207	49	4:1	191	52	3:1
Jumla	**1118**	**204**	**5:1**	**1302**	**203**	**6:1**

Bunda

	2015			2016		
Darasa	Wanafunzi	Walimu	Jumla	Wanafunzi	Walimu	Uwiano
Kidato cha 1	1228	75	16:1	1788	93	19:1
Kidato cha 2	995	78	12:1	1087	86	12:1
Kidato cha 3	1096	80	13:1	638	84	7:1
Kidato cha 4	1102	80	14:1	997	93	11:1

Kigoma vijijini

Mwaka	2015			2016		
	Wanafunzi	Walimu	Uwiano	Wanafunzi	Walimu	Uwiano
Kidato cha 1	573	84	7:1	804	88	9:1
Kidato cha 2	671	90	7:1	579	82	7:1
Kidato cha 3	637	93	7:1	513	82	6:1
Kidato cha 4	730	85	9:1	459	82	6:1

Magu

Shule	2015			2016		
	Wanafunzi	walimu	uwiano	wanafunzi	walimu	uwiano
Lubugu	563	34	1:17	612	35	1:17
Magu	1031	51	1:20	1030	51	1:20
Kinago	962	35	1:27	1088	34	1:32
Itumbili	887	35	1:25	547	35	1:16
Sukuma	540	30	1:18	601	28	1:21
Ng'haya	520	31	1:17	571	29	1:20
Mugini	94	12	1:9	136	12	1:11
Kahangara	531	33	1:16	560	35	1:16
Kandawe	481	44	1:11	524	40	1:13
Ng'wamabanza	296	32	1:9	298	30	1:10

Kishapu

Mwaka	2015				2016			
Shule	Kidato cha 1	Kidato cha 2	Kidato cha 3	Kidato cha 4	Kidato cha 1	Kidato cha 2	Kidato cha 3	Kidato cha 4
Ufundi Mwadui	1:16	1:11	1:13	1:12	1:20	1:13	1:13	1:11
Kishapu	1:117	1:88	1:91	1:112	1:105	1:119	1:70	1:84
Maganzo	4:182	2:108	2:100	2:100	5:238	3:138	1:75	1:78
Mwigumbi	1:61	1:58	1:58	1:41	1:97	1:64	1:50	1:56
Mangu	1:8	1:5	1:5	1:6	1:13	1:7	1:4	1:5
Mwataga	1:24	1:24	1:14	1:8	1:30	1:19	1:24	1:21
Mwamaduli	1:29	1:22	1:19	1:15	1:32	1:26	1:21	1:18
Uchunga	1:30	1:34	1:28	1:27	1:30	1:30	1:34	1:28
Idukilo	1:77	1:53	1:44	1:36	1:121	1:55	1:46	1:40
Bunambiyu	1:77	1:08	1:09	1:09	1:22	1:15	1:09	1:09

Mufindi

Wilaya / Halmashauri	2015			2016		
	Wanafunzi	Walimu	Uwiano	Wanafunzi	Walimu	Uwiano
Mufindi	504	44	11:1	581	45	13:1
Mufindi	537	44	12:1	545	45	12:1
Mufindi	299	44	7:1	465	45	10:1
Mufindi	414	44	9:1	278	45	6:1
Jumla	**1754**	**176**	**10:1**	**1869**	**180**	**10:1**

Mafinga Mji

Wilaya / Halmashauri	2015			2016		
	Wanafunzi	Walimu	Uwiano	Wanafunzi	Walimu	Uwiano
Mafinga Mji	802	100	8:1	994	102	10:1
Mafinga Mji	973	100	10:1	838	100	8:1
Mafinga Mji	747	97	8:1	863	99	9:1
Mafinga Mji	757	101	7:1	556	97	6:1
Jumla	**3279**	**398**	**8:1**	**3251**	**398**	**8:1**

Kwa mujibu wa takwimu hapo juu, hali ya uwiano wa walimu kwa idadi ya wanafunzi katika shule ambazo zimefanyiwa utafiti unaonyesha kuwa ni mzuri kwenye baadhi ya Wilaya/ Halmashauri na baadhi yake kutokuwa mzuri. Hii inamaanisha kuwa juhudi za makusudi zinahitajika ili kufikia uwiano wa 20:1 kufikia mwaka 2020/21 na 2025/26. Wilaya/Halmshauri zenye uwiano mzuri zinachagizwa na uwepo wa idadi kubwa ya walimu wa masomo ya sanaa (Arts) kuliko masomo ya Sayansi. Mfano Wilaya Kishapu; Kuna uhitaji mkubwa wa walimu wa hisabiti na sayansi kwa ujumla. Zaidi ya walimu 32 walihama mwaka 2016 hii ni sawa na ongezeko la 1% ya upungufu wa walimu wanaohitajika katika wilaya ya Kishapu. Utafiti umebaini kuwa wastani wa mwalimu mmoja hufundisha wanafunzi mia moja na mbili 1:102, hii ni kinyume na sera na Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa. Na katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma Vijijini uwiano wa walimu na masomo ya sayansi ni 1:200 kwa mujibu wa takwimu za utafiti huu. Mfano; Shule ya Sekondari Mkigo, Kigoma vijijini ikiwa haina mwalimu hata mmoja wa masomo ya sayansi. Juhudi za makusudi hasa kwa upande wa serikali kuweza kuajiri walimu wa masomo ya sayansi na masomo mengine ili kukabiliana na changamoto hii.

3.7. Uwiano wa wanafunzi na Matundu ya vyoo

Serikali imekusudia kufikisha uwiano wa 20:1 mwaka 2020/21 na 2025/26 kutoka 29:1 mwaka 2014/15. Taarifa hapa chini zinaonyesha hali halisi iliyopo katika ngazi ya Wilaya/ Halmashauri na katika ngazi ya shule kwa mujibu wa utafiti huu.

Ngazi ya Wilaya/Halmashauri

Halmashauri ya Mufindi

Mwaka	2015		2016	
Jinsia	Me	Me	Me	Ke
Wanafunzi	5697	6035	5677	5978
Matundu ya vyoo	316	334	324	341
Uwiano	1:18	1:18	1:18	1:18

Mafinga Mji

Mwaka	2015		2016	
Jinsia	Me	Ke	Me	Ke
Wanafunzi	2267	2153	2093	2111
Matundu ya Vyoo	103	101	91	97
Uwiano	1:22	1:21	1:23	1:22

Rungwe

Mwaka	2015		2016	
Jinsi	Me	Ke	Me	Ke
Wanafunzi	7,841	7257	7602	7139
Vyoo	337	339	241	279
Uwiano	1:23	1:21	1:31	1:26

Kigoma Vijijini

Mwaka	2015		2016	
Jinsi	Me	Ke	Me	Ke
Wanafunzi	3677	1849	3463	1951
Matundu ya vyoo	129	103	129	103
uwiano	1:4	1:6	1:4	1:5

Kishapu

Mwaka	2015		2016	
Jinsi	Me	Ke	Me	Ke
Wanafunzi	4551	2572	4794	3423
Vyoo	89	92	116	119
Uwiano	51:1	27:1	41:1	28:1

Ngazi ya Shule

Bunda

Shule	2015			2016		
	Wanafunzi	Matundu	Uwiano	Wanafunzi	Matundu	Uwiano
Nyiendo-Me	424	5	84:1	424	5	84:1
Nyiendo-Ke	379	6	63:1	379	6	63:1
Sizaki-Me	194	8	24:1	195	8	24:1
Sizaki-Ke	140	7	20:1	140	7	20:1
Kabasa-Me	27	1	27:1	21	1	21:1

Kabasa-Ke	35	1	35:1	26	1	26:1
Wariku-Me	208	4	52:1	204	4	51:1
Wariku-Ke	107	4	26:1	117	4	29:1
Mihingo-Me	79	6	13:1	88	6	14:1
Mihingo-Ke	23	6	3:1	12	6	2:1
Mekomarilo-Me	92	4	23:1	83	4	20:1
Mekomarilo-Ke	58	4	14:1	64	4	16:1
Chamriho-Me	180	8	22:1	235	8	29:1
Chamriho-Ke	139	8	17:1	181	8	22:1
Guta-Me	291	9	32:1	287	9	31:1
Guta-Ke	155	9	17:1	163	9	18:1
Muranda-Me	315	14	22:1	397	14	28:1
Muranda-Ke	194	8	24:1	300	8	37:1
Chitengule-Me	520	8	65:1	479	8	59:1
Chitengule-Ke	297	8	37:1	322	8	40:1
Jumla	**3857**	**128**	**30:1**	**4117**	**128**	**32:1**

Kishapu

Mwaka	**2015**			**2016**		
Shule	**Me**	**Ke**	**Vyoo**	**Me**	**Ke**	**Vyoo**
Ufundi Mwadui	198	156	8	191	197	8
Kishapu			8			8
Maganzo	232	252	6	247	276	6
Mwigumbi	111	107	6	124	136	6
Mangu	111	140	10	166	173	10
Mwataga	110	99	6	149	113	6
Mwamaduli	150	105	5	169	119	5
Uchunga	107	112	6	109	131	6
Idukilo	115	91	6	148	123	6
Bunambiyu	180	124	2	232	174	2
Jumla	**1314**	**1186**	**63**	**1535**	**1442**	**63**

Rungwe

Mwaka	**2015**		**2016**		**2015**				**2016**			
Jinsi	**Me**	**Ke**	**Me**	**Ke**	**Me**	**uwiano**	**Ke**	**uwiano**	**Me**	**uwiano**	**Ke**	**uwiano**
Mpuguso	444	502	429	458	18	24:1	18	28:1	18	24:1	18	25:1
Bujinga	422	441	411	446	15	28:1	15	29:1	15	27:1	15	30:1
Kyimo	245	278	240	270	10	26:1	8	35:1	10	24:1	8	34:1
Tukuyu	269	327	231	244	17	16:1	15	22:1	17	14:1	15	16:1
Isongole	314	316	299	306	13	24:1	16	20:1	13	23:1	16	19:1
Ilima	170	148	142	141	8	21:1	6	25:1	8	18:1	6	24:1
Kiwira	0	0	0	0	16	0	16	0	16	0	16	0
Mpandapanda	322	323	322	300	4	80:1	8	40:1	4	81:1	8	38:1

Takwimu hapo Juu zinaonyesha kuwa juhudi za ziada zinahitajika ili kuweza kufikia uwiano wa 20:1 kwa mujibu wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa 2020/21. Hali ya vyoo imekuwa na athari kubwa kwa wanafunzi hasa kwa watoto wa kike hasa vinapokuwa havitoshi kwa idadi ya wanafunzi lakini pale vinapokuwa havina usafi unaotakiwa. Hali haiwezi kuwa shwari pale uwiano unapokuwa 50:1 au kwa 61:1 katika shule zetu. Idadi ya matundu ya vyoo ni lazima iongezwe lakini pia usafi wa vyoo hivyo ni lazima uzingatiwe.

Hali ya Miundombinu ya Vyoo Katika Maeneo Mbalimbali

Picha Juu: Vyoo vya Shule ya Sekondari Ilima Rungwe, vikiwa havina Milango

Picha Juu: Choo cha Walimu na Wanafunzi Shule ya Sekondari ya Kineng'ene, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi

Picha Juu: Choo cha wavulana, Shule ya Sekondari Muranda, Bunda

Picha Juu: Vyoo vya ndani ya bweni la wasichana la shule ya Sekondari Mnyigumba, Mufindi – Iringa likiendelea kukamilishwa. Huu ni mfano mzuri wa kuigwa. Kuwa na mazingira bora na salama kwa ajili ya Elimu hasa kwa wanafunzi wa jinsi ya kike.

Miundombinu Mingine

Picha Juu: Nyumba ya walimu Shule ya Sekondari Mkigo, Kigoma vijijini. Nyumba hii yenye vyumba vitatu inakaliwa na walimu watano (5) pamoja na familia zao.

MAONI YA WADAU

BODI ZA SHULE, WALIMU, WAZAZI, KAMATI ZA MAENDELEO YA KATA NA WANAFUNZI

CHANGAMOTO ZA UPATIKANAJI WA ELIMU

- Uhaba wa hosteli kwa ajili ya wanafunzi wa kike
- Uhaba wa walimu hasa walimu wa masomo ya sayansi
- Maabara nyingi hazijakamilika
- Upungufu wa vifaa vya maabara, madawati na nyumba za walimu
- Shule kukosa maji na umeme
- Wazazi hawashiriki katika maendeleo ya shule hasa baada ya tamko la elimu bure.
- Mila na jadi potofu kwa watoto wa kike (ikiwemo Tohara, kuozwa ikiwa ni sehemu ya kujipatia kipato)
- Wanafunzi wa kike kuwa sehemu kubwa ya usaidizi wa kazi za nyumbani hivyo kukosa muda wa kutosha ya kujisomea wakiwa nyumbani.
- Walimu kuwarubuni wanafunzi wa kike
- Umbali wa kufikia shule huwapa vishawishi vya kuingia katika mahusiano; Mfano boda boda
- Kukosa huduma ya chakula cha mchana huathiri masomo ya wanafunzi
- Utoro mashuleni
- Athari za utekelezaji wa tamko la elimu bila malipo shuleni (waraka wa elimu na.5 wa 2015) waraka huo umeandaliwa katika namna ambayo inamfanya mzazi ajivue jukumu la kuchangia maendeleo ya elimu ya mwanae, wakati uhalisia wa fedha za ruzuku kwa ajili ya kuendeshea shule hazitoshi kukidhi mahitaji ya shule kwa wakati.
- Ukame umepelekea watoto kutokuja shule kwani sehemu kubwa ya wazazi hawana chakula na watoto wa kike kubaki nyumbani kusaidia utafuta maji siku nzima
- Kamati ya Maendeleo ya Kata kuwa na mamalaka ya kubadilisha matumizi ya pesa kupeleka matumizi sehemu ambazo si kipaumbele cha shule.

NINI KIFANYIKE

- Walimu waongezwe mashuleni hasa wa masomo ya Sayansi
- Wanafunzi wajengewe hosteli haswa wanafunzi wa jinsi ya kike, itawaepusha na mila potofu na vishawishi
- Shule pamoja na wazazi zianzishe utaratibu wa chakula cha mchana kwa wanafunzi wa kutwa
- Wazazi kwa kila shule wahamasishwe kushiriki ujenzi wa vyumba zaidi vya madarasa, ujenzi wa maabara na ujenzi wa hosteli/mabweni ili wanafunzi wasitembee umbali mrefu
- Katika vikundi vya majadiliano, wanafunzi pia waliomba wadau wa elimu watoe elimu kwa wazazi ili kuwajengea uwezo wa kutambua nafasi zao ili waweze kushirikiana na Walimu na wadau wengine wa elimu katika kujiletea mafanikio na maendeleo shuleni
- Nyumba za walimu na vifaa vya maabara viongezwe
- Shule zijengewe miundombinu ya maji na umeme

Baadhi ya watafiti wetu katika vikundi vya Majadiliano na Maeneo mengine ya Tafiti.

SHULE YA SEKONDARI YA GUTA

Shule ya sekondari ya Guta – Kata ya Guta katika vikundi vya Majadiliano na Mtafiti wetu Mama Verena Materego

Shule ya sekondari Mkigo (Kigoma) – Wanafunzi na Benedict Mosha (Mtafiti) katika mahojiano

Shule ya sekondari Mnyigumba, Mufindi – Iringa. Mtafiti wetu Ndugu Charles Lwabulala akitembelea Bweni la Wasichana likiwa linaendelea na ujenzi pamoja na jiko (Picha Kulia) linalotumika hivi sasa.

TANZANIA COALITION ON DEBT AND DEVELOPMENT (TCDD)

Shaurimoyo Road, Ilala Area, Mariam Tower, 7th Floor
P.O. Box 80147, Dar es Salaam, Tanzania.

Tel: +255 22 2866866 **Mobile:** +255 736 502661
E-mail: ttcdd@yahoo.com or info@tcdd.or.tz
Website: www.tcdd.or.tz